# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 22 Mei, 2023**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

107. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na msisitizo mkubwa wa Serikali juu ya kutunza usafi na mazingira yanayotuzunguka katika visiwa vyetu. Hata hivyo, juhudi na rasilimali nyingi zimekuwa zikielekezwa kwenye maeneo ya mjini huku sehemu za vijijini zikiachwa zijiendeshe wenyewe na kujitegemea kirasilimali na nyenzo.

(a) Je, ni ipi hali ya rasilimali ya vikundi vya usafi na mazingira vya shehia katika sehemu za vijijini.

(b) Je, Serikali inavisaidia vipi vikundi vya usafi na mazingira katika shehia.

(c) Je, vikundi vya usafi na mazingira katika shehia vinadhibitiwa na kukaguliwa na nani ili kuhakikisha kwamba hawatendi mambo nje ya majukumu yao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

28. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa maji ni uhai kwa viumbe na mimea na ni muhimu kwa maisha ya binadamu na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Na kwa kuwa jimbo la Kojani limekumbwa na upungufu mkubwa wa maji kwa matumizi ya kawaida na hata kwa matayarisho ya ibada katika misikiti mbali mbali.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizoikwaza Wizara yako hata ikapelekea kuwepo kwa shida na dhiki hii katika jimbo la Kojani.

(b) Ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italitatua tatizo la maji katika jimbo la Kojani.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

128. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Uwekezaji wenye viwango vya kimataifa unatarajiwa kuiinua Zanzibar kiuchumi. Hata hivyo, matayarisho bado hayajaridhisha katika kuvutia wawekezaji wakubwa wa nyanja tofauti.

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika kuanzisha vituo vya maonesho, mikutano na biashara (Exhibitions, Convention and Trade Centres) ili kuvutia wawekezaji wakubwa.

(b) Je, ni kwa kiasi gani Wazanzibari wana uweledi wa kutoa huduma katika vituo vya maonesho, mikutano na biashara (Exhibitions, Convention and Trade Centres) vitakavyowavutia wawekezaji wakubwa wa kimataifa.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuwapa mafunzo maalum Wazanzibari, ili waweze kutoa huduma bora za uwekezaji kwa uweledi badala ya kuwalalamikia kwamba hawana uwezo na nafasi muhimu kujazwa na wasiokuwa Wazanzibari.

**Wizara ya Afya:**

43. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ndiyo tegemezi katika kutoa huduma bora za afya hapa Zanzibar. Na kwa kuwa baadhi ya hospitali kubwa nchini zimeanzisha huduma ya kutoa kozi (program) mbali mbali za afya ambapo pia huchangia mapato ya nchi.

(a) Je, Wizara ya Afya kupitia Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja inalionaje wazo hilo la kuanzisha "program" za mafunzo ya afya (Diploma na Shahada).

(b) Je, ni lini Wizara yako itaanzisha mpango huo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

9. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa zoezi la uwekaji namba katika nyumba lilifanyika vyema na kupiga hatua nzuri wakati wa maandalizi ya sensa. Na kwa kuwa zoezi hili limesita kwa sasa na linaonekana kama kwamba limeisha wakati zipo nyumba ambazo wamiliki wake wamelipa, bila ya kuwekewa namba hizo huku ikionekana wazi kuwa hakuna muendelezo wa zoezi hili. Na kwa kuwa zoezi hili ni muhimu kwa ajili ya utambuzi wa anuwani za nyumba na majengo yetu kuweza kutumika kwa njia mbali mbali kama vile huduma za posta na biashara za mtandaoni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha zoezi hili linakuwa endelevu na kuleta tija iliyokusudiwa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

119. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na utaratibu usioridhisha wa wazazi wa wanafunzi wa vyuo wanaohitaji wakalimani kulazimika kuwatafuta wakalimani hao na kulipia huduma ya ukalimani wenyewe kwa ajili ya huduma hiyo kwa watoto wao ambao ni wanafunzi halali wa vyuo husika na wana mahitaji maalumu kama walivyoyaainisha wakati wanaomba nafasi za masomo katika

vyuo hivyo.

(a) Je, ni utaratibu upi rasmi uliowekwa na Serikali kuhusiana na kuwawekea mazingira rafiki wanafunzi wa vyuo wanaohitaji ukalimani wakiwa darasani.

(b) Je, ni zipi haki za msingi za wanafunzi hawa kuhusiana na kupatiwa wakalimani na vyuo husika au Serikali.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuwa na muongozo ulio wazi na rasmi wa kuzielekeza taasisi zinazotoa elimu kuhusiana na ulazima wa kuwa na wakalimani, kama wafanyakazi rasmi wa taasisi hizo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

56. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Suala la mipango miji ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu ingawa inaonekana wazi kuwa bado hatujafanikiwa kwenye jambo hili.

(a) Je ni sababu zipi zinazopelekea ugumu huu.

(b) Ni upi mpango wa Serikali kwa tunakoelekea katika suala zima la mipango miji.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

65. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kilimo cha maweni (juu) ni kilimo kinachohitaji gharama kubwa wakati wa kutayarisha shamba kwa ajili ya kupanda mazao, hasa viazi vikuu, muhogo na mazao mengine.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa maweni kupata mbolea japo kwa gharama nafuu.

II. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
22 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA